ROMAN CATHOLIC DIOCESE OF NJOMBE
LUGARAWA HEALTH TRAINING INSTITUTE (LUHETI)
*(Quality Education – Quality Service)*
P.O Box 389 NJOMBE, TEL. +255 758646807
Email: principal@luheti.ac.tz
**NJOMBE, TANZANIA.**



**MUUNDO WA ADA (FEE STRUCTURE) KOZI YA MAABARA YA SAYANSI TIBA (UP-GRADING MEDICAL LABORATORY SCIENCES) KWA MWAKA WA MASOMO WA 2024/2025**

## MAELEZO KWA UJUMLA:

- Malipo yote yafanyike kupitia **Benki ya CRDB**, akaunti za chuo zimeainishwa kwenye jendwali linaloonesha namna malipo yanavyo fanyika na utawasilisha risiti halisi chuoni ofisi ya Muhasibu.
- Ufikapo chuoni unatakiwa uwe umelipa ada kama ilivyoainishwa kwenye jedwali **namba 04** na michango ya mwaka husika kama ilivoainishwa kwenye jedwali **namba 05.**
- Ada haitabadilika katikati/ndani ya mwaka wa masomo, lakini inaweza kubadilika mwanzo wa mwaka wa masomo unaofuata hii inategemeana na mabadiliko ya gharama ya kuendesha mafunzo.
- Sare: Kaunda suti-1, gauni-1 na T-shirt 1 vyote vinapatikana chuoni. Ikiwa mwanafunzi atatahitaji kuongeza jozi nyingine ya sare atapaswa kushona kulingana na muongozo uliowekwa utakao patikana katika ofisi ya malezi ya wanafunzi.
- Mwanafunzi atajitegemea chakula ambacho kinapatikana katika cafeteria ya chuo kwa bei nafuu.
- Kabla ya kufika chuoni kila mwanafunzi atapaswa kufanyiwa uchunguzi wa kiafya na kujaza fomu maalumu ya kitabibu (Medical Examination Form)
- Wanafunzi wote wa mwaka wa kwanza watalazimika kuishi katika hosteli za chuo
- Mwanafunzi wa mwaka wa pili na wa tatu anaruhusiwa kuishi kwenye hosteli zilizopo ndani na nje ya chuo.
- Gharama ya utafiti kwa mwanafunzi wa mwaka wa tatu atajitegemea
- Endapo mwanafunzi atafeli mtihani wa majaribio gharama ya kurudia mtihani huo ni Tsh. 10,000/= kwa kila somo la nadharia na Tsh. 10,000/= kwa somo la vitendo. Endapo atafeli nadharia na vitendo gharama ya kurudia mitihani hiyo ni Tsh 20,000/=.
- Endapo mwanafunzi atafeli mtihani wa kumaliza muhula wa kwanza au wa pili, gharama ya kurudia mtihani huo ni Tsh. 100,000/= bila kujalisha idadi ya masomo aliyofeli.
- Endapo mwanafunzi hatofanya mtihani pale unapofanyika kwa mara ya kwanza na akaomba kufanya mtihani maalumu (special examination), gharama ya kufanya mtihani huo ni Tsh. 50,000/= bila kujalisha idadi ya masomo aliyofeli.
- Wanafunzi wote wanapaswa kuwa wanachama hai wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) au bima nyingine ya afya inayokubalika katika hospitali za umma na binafsi. Kwa wanafunzi wasio na bima hai za afya, watapaswa kuchangia kiasi cha Tsh. 50,400 kila mwaka.
- Kwa wanafunzi watakao wasilisha maombi ya kujiunga na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), kadi zao za bima zitakuwa tayari ndani ya siku thelasini (30) tangu kusajiliwa chuoni na kuwasilisha maombi hayo. Kila mwanafunzi aliyefikia umri wa miaka 18 anatakiwa kuwa na Namba ya kitambulisho cha Taifa (NIDA) kwa ajili ya usajili wa Bima ya Afya (NHIF)

## MAHITAJI BINAFSI YA MSINGI

- Shuka 4, blankenti 1, mto na foronya, taulo, nguo za michezo, sweta lenye rangi nyeupe isiwe na maandishi, ndoo ya kuogea, chandarua, soksi nyeupe kwa wasichana, soksi nyeusi kwa wavulana, viatu vyeusi, viwe vya kufunika miguu na sio vya mikanda (open shoes) Pia visiwe vyenye visigino virefu na vinavyopiga kelele wakati unapotembea.
- Kuwa na fedha za matumizi madogo madogo ukiwa hapa chuoni pamoja na chakula

## NAMNA YA KUFIKA CHUONI

Chuo kinapatikana mkoa wa Njombe wilaya ya Ludewa- Lugarawa, kwa wanaotoka mikoani fika Stendi kuu ya mabasi Njombe, panda gari za kuelekea Lugarawa, ukifika Lugarawa shuka kituo cha **Junction** au **Hospitali ya St. John's Lugarawa**.

## SEHEMU A: GHARAMA ZA MAFUNZO-MAABARA YA SAYANSI TIBA (UP-GRADING MEDICAL LABORATORY SCIENCES) KWA MWAKA WA MASOMO WA 2024/2025

### JEDWALI NAMBA 01: ADA NA MICHANGO MINGINE YA CHUO

| N a. | MAELEZO | KIASI (TSH) |
|---|---|---|
| 1. | **Ada (Tuition fee)** | **1,200,000** |
| | | |
| | **MICHANGO MINGINE** | |
| 1. | Mitihani ya ndani | 150,000 |
| 2. | Usajili | 20,000 |
| 3. | Cheti cha kuhitimu (Leaving Certificate) | 20,000 |
| 4. | Huduma za Maktaba | 20,000 |
| 5. | Mahafali (pamoja na Joho) | 85,000 |
| 6. | Mafunzo kwa vitendo (Field work practice) | 200,000 |
| 7. | Usimamizi wa utafiti (Research supervision) | 50,000 |
| 8. | Michezo | 10,000 |
| 9. | Fedha ya uendeshaji wa serikali ya wanafunzi (Luheti Student Organisation Fee) | 10,000 |
| 10. | Kitambulisho | 10,000 |
| 11. | Vitabu vya mazoezi | 80,000 |
| 12. | Sare(Gauni-1, suruali&shirt-1,T-shirt 1), Laboratory coat | 95,000 |
| 13. | Hospital clinical rotations | 200,000 |
| | **Jumla Kuu** | **2,150,000** |

### JEDWALI NAMBA 02: MICHANGO MAALUMU

| S/N | Maelezo | KIASI (TSH) |
|---|---|---|
| 1 | NACTVET Quality assurance | 15,000 |
| 2 | Ada ya mitihani ya Wizara ya Afya | 150,000 |
| 3 | Mchango wa CSSC | 5,000 |
| | **Jumla** | **170,000** |

### JEDWALI NAMBA 03: JUMLA YA ADA NA MICHANGO YOTE NA NAMNA YA KULIPA

### JEDWALI NAMBA 03: JUMLA YA ADA NA MICHANGO

| MUHULA | MWAKA III |
|---|---|
| MUHULA WA I | 1,235,000 |
| MUHULA WA II | 1,085,000 |
| **JUMLA KUU** | **2,320,000** |

## SEHEMU B: VIFAA VYA KUTUMIA WAKATI WA MAFUNZO

i) Madaftari makubwa (counterbooks) Quire 2 yasiyopungua Matano (5)
ii) Clean gloves 1 box (examination gloves) kila anapoanza mwaka wa masomo
iii) Improved neubauer chamber (haemocytometer) -1
iv) White gumboot

**JEDWALI NAMBA 04: MALIPO YA ADA**

| NAMNA YA KULIPIA ADA | MWAKA III |
|---|---|
| **MUHULA WA KWANZA** | |
| AWAMU –1<br>1/10/2024 | 300,000 |
| AWAMU – 2<br>1/1/2025 | 300,000 |
| **MUHULA WA PILI** | |
| AWAMU – 3<br>1/4/2025 | 300,000 |
| AWAMU – 4<br>1/6/2025 | 300,000 |
| **JUMLA** | **1,200,000** |
| ***CRDB BANK,***<br>***Jina la Akaunti: LUGARAWA HEALTH TRAINING INSTITUTE***<br>**0150219983400** | |

**JEDWALI NAMBA 05: MALIPO YA MICHANGO**

| NAMNA YA KULIPIA MICHANGO | MWAKA III |
|---|---|
| **MUHULA WA KWANZA** | |
| AWAMU –1<br>1/10/2024 | 400,000 |
| AWAMU – 2<br>1/1/2025 | 235,000 |
| **MUHULA WA PILI** | |
| AWAMU – 3<br>1/4/2025 | 485,000 |
| **JUMLA** | **1,120,000** |
| ***CRDB BANK,***<br>***Jina la Akaunti: LUGARAWA HEALTH TRAINING INSTITUTE***<br>**015C219983400** | |

***NB:***

- ***i.*** ***Ndugu Mzazi /Mlezi/Mfadhili hakiki akaunti vizuri kadili ya jedwali lilivyoainisha***
- ***ii.*** ***Akaunti zote mbili ni za CRDB BANK na zote zinasomeka Jina la: LUGARAWA HEALTH TRAINING INSTITUTE***
- ***iii.*** ***FEDHA IKIWEKWA KWENYE AKAUNTI HAIREJESHWI***

..............................................

**Buteye D. Buteye**

**MKUU WA CHUO**

LUGARAWA HEALTH TRAINING INSTITUTE
PRINCIPAL
20 MAY 2024
(LUHETI)
P. O. BOX 389, NJOMBE